



What do I need to know if my child gets a formal caution?

Parent/carer information

Ninahitaji kujua nini ikiwa mtoto wangu anapata tahadhari rasmi?

Habari kwa mzazi/mlezi

Je, tahadhari rasmi kwa tabia ya wasiwasi ni nini?

Tabia mbaya ya wasiwasi ni kitu ambacho mtu hufanya kinachoweza kusababisha au kimesababisha madhara au hatari kwake mwenyewe au kwa wengine. Tahadhari rasmi inamwambia mwanafunzi kwamba tabia zake zilisababisha au zinaweza kusababisha madhara au hatari kwake mwenyewe na kwa watu wengine. Imeundwa ili kukujulisha wewe na mtoto wako kwamba tabia zake zinahitaji kuboreshwa.

Tahadhari rasmi ni barua ambayo tabia ya wasiwasi ya mtoto wako imerekodiwa. Mtoto wako hatasimamishwa kwa wakati huu.

Je, nini inatokea kama mtoto wangu anapata tahadhari rasmi?

Shule itajadili tabia mbaya zile za wasiwasi na kueleza tahadhari rasmi kwa mtoto wako. Mkuu wa shule pia atakupa nakala iliyoandikwa ya tahadhari rasmi.

Lengo la tahadhari rasmi ni kukupa wewe na mtoto wako muda wa kuelewa athari za tabia zake na kukubali juu ya mpango wa msaada wa kushiriki katika mikakati ya kusaidia tabia nzuri. Shule itakupa wewe na mtoto wako nafasi ya kukutana nao kujadili tabia na kupanga au kukagua misaada ambayo mtoto wako anahitaji.

Unaweza kuja na [mtu wa usaidizi](#) pamoja nawe kwenye mikutano yoyote na shule.

Tahadhari rasmi iko kwa hadi siku 50 za shule. Wakati wa kipindi hiki, mtoto wako anaweza kusimamishwa kama tabia ikitokea tena au kwa sababu ya tabia mbaya nyingine.

Je, nitafanyaje ikiwa mtoto wangu anapata tahadhari rasmi?

Karibu kila mtoto wakati mwingine atafanya mambo ambayo hayafuati sheria za shule au [Kanuni ya Tabia kwa Wanafunzi](#). Wakati mwingine, inapotokea, tahadhari rasmi atapewa. Habari zaidi juu ya [nini cha kufanya kama mtoto wako anapata shida shuleni](#) inapatikana.

Ikiwa mtoto wako anapokea tahadhari rasmi, ina maana kuwa kuna tabia inayohitaji umakini. Kushiriki kwako na shule ni muhimu sana katika kudhibiti tabia ya mtoto wako na kutayarisha masuluhisho pamoja. Ongea na mkuu wa shule kuhusu tahadhari rasmi na ushirikiane na timu inayomsaidia mtoto wako kupata masulisho fulani.

Itakuwaje kama tabia inatokea tena?

Ikwia tabia ya wasiwasi ikitokea tena katika siku 50 za shule za tahadhari rasmi ya asili, mkuu anaweza kuamua kusimamisha mtoto wako. Uamuzi wa kusimamisha mtoto wako utatokea tu baada ya mkuu anaangalia tabia hiyo, na mahitaji binafsi ya mtoto wako na watoto wengine. Habari juu ya [kusimamisha mwanafunzi](#) inapatikana.

Nifanye nini ikiwa bado nina wasiwasi yoyote?

Ikiwa una wasiwasi kuhusu ujifunzaji, tabia au ustawi wa mtoto wako shuleni, mahali pazuri pa kuanza ni kuzungumza na mwalimu, mkuu msaidizi au naibu mkuu. Masuala mengi yanaweza kutatuliwa kwa kujadiliana na watu wanaomjua mtoto wako na hali hiyo.

Wakati mwingine unaweza kuhitaji kuongea na mtu mwingine. Shule yako inaweza kukupa habari ya mawasiliano kwa ofisi ya elimu ya mtaa wako huenda anayeweza kusaidia. Pia fikiria kuzungumza na daktari wa mtoto wako kama ukiona kungeweza kuwa sababu ya matibabu kwa wasiwasi yako.

Habari zaidi kuhusu [kutetea kwa ajili ya mtoto wako](#) inapatikana, pamoja na [Mkatamba wa Jamii ya Shule](#) ambao unaeleza njia za kuwasiliana na shule.

Ninaweza kupata habari gani kutoka shule?

Unaweza kuuliza shule kukupa habari zaidi kuhusu ile ilichotokea na kwa nini. Shule inapaswa kukueleza kwako sababu za maamuzi yoyote, hatua gani ambazo zitatokea na nini cha kufanya kama una suala.

Huduma ya mkalimani wa simu

Ikiwa unataka kuwasiliana na shule na unahitaji usaidizi na Kiingereza tafadhali piga simu kwa huduma ya mkalimani wa simu kwenye 131 450, umwambie lugha gani unayohitaji na mwombe mpigaji simu kupiga simu shuleni. Mpigaji simu atapata mkalimani kwenye simu kukusaidia na mazungumzo yako. Hutatozwa kwa huduma hii.